## WIZARA YA ELIMU NA UTAMADUNI

# SERA YA MAENDELEO YA MICHEZO

# SERA YA MAENDELEO YA MICHEZO

## YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| 1. | Utangulizi | 1 |
| 2. | Madhumuni ya Sera | 8 |
| 3. | Vyombo vyenye jukumu la kutekeleza Sera | 10 |
| 4. | Utaratibu na uendeshaji wa Michezo mbalimbali | 27 |
| 5. | Mafunzo kwa Wanamichezo | 35 |
| 6. | Uteuzi wa Timu za Taifa | 38 |
| 7. | Huduma za Wanamichezo | 40 |
| 8. | Ujenzi na utunzaji wa Viwanja vya Michezo | 33 |
| 9. | Vyombo vya Habari katika Kuendeleza Michezo | 42 |
| 10. | Ugharamiaji wa Michezo | 43 |
| 11. | Viambatisho: | 45 |

(i) Orodha ya Vyama vya Michezo
(ii) International Charter of Physical Education and Sport.

# DIBAJI

Nchi haiwezi kutambulika kama taifa huru bila kuwa na utamaduni wake. Mojawapo ya viungo muhimu katika utamaduni wa kila jamii ya binadamu duniani ni michezo. Michezo ni chombo muhimu sana katika kuendeleza jamii. Aidha michezo huweza kuwa kielelezo na utambulisho wa taifa kwa kutoa burudani, kujenga na kukomaza afya ya mwili na akili, kujenga nidhamu, kujitangaza kiuwezo na vipaji nchi inaposhiriki katika michezo ya kimataifa na hivyo kulitangaza taifa linalohusika.

Kutokana naumuhimu wa michezo kwa jamii katika kila kipindi cha historia ya binadamu Watanzania nao pia walikuwa wakishiriki katika michezo mbalimbali katika makabila yao. Michezo hiyo ni kama vile mieleka, kulenga shabaha ya upinde na mishale na kuogelea. Michezo hii ambayo ilijenga kujiamini na kuwa utambulisho wa jamii inaitwa kwa jumla **michezo ya jadi**. Kwa bahati mbaya michezo hii haikupewa msukumo uliostahili baada ya kuja kwa wakoloni. Kutokana na kutotiliwa maanani michezo hii ilififia. Badala yake, wakoloni waliingiza michezo ya kigeni ambayo wao waliifahamu. Michezo hii mipya ni kama vile mpira wa miguu, netiboli, ndondi, mpira wa meza, mpira wa mikono na mbio za baiskeli. Baadhi ya michezo hii kama

vile mpira wa miguu ilienea sana na kupendwa sana na wananchi.

Baada ya nchi yetu kupata uhuru, Serikali mpya ya wananchi iliitambua michezo kuwa ni sehemu ya uhai na utashi wa taifa letu. Serikali iliunda Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana mwaka 1962 ambayo, pamoja na majukumu yake mengine, ilipewa jukumu la kusimamia maendeleo ya michezo. Tangu wakati huo nchi yetu imepata mafanikio katika mpira wa miguu, riadha, ndondi, netiboli na michezo mingineyo. Mbali na mafanikio hayo imedhihirika kwamba wapo Watanzania wengi wenye vipaji ambao vipaji vyao vikiendelezwa nchi yetu inaweza kufikia kiwango cha juu sana katika michezo ya kimataifa. Nivigumu kuendeleza vipaji hivi bila ya nchi kuwa na Sera. Kutokana na Serikali kutambua ukweli huu ndipo ilipoandaa **Sera** hii ili iwe dira ya uendeshaji na uendelezaji wa michezo katika nchi yetu.

Madhumuni ya **Sera** hii yameelezwa bayana, na kazi za vyombo vinavyosimamia maendeleo ya michezo yameelezwa ili kuondoa utata katika utekelezaji. Kwa mfano, kazi za Wizara yenye dhamana ya kuendeleza michezo, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Mabaraza ya Michezo ya Mikoa na Wilaya zimeelezwa kwa ufasaha.

Maendeleo ya michezo yanagusa na kutegemea juhudi za Wizara nyingine nyingi. Wizara hizi nazo zimetajwa pamoja na majukumu ambayo zinatarajiwa kuyatimiza. Kuhusu maswali mengi ambayo yalikuwa yanaulizwa na wale wote wenye nia ya kuendeleza michezo bila kupata majibu ya uhakika sasa yamefafanuliwa. Kwa mfano, **Sera** inapendekeza mbinu za kuendeleza michezo ya jadi, ikiwa ni pamoja na kuifanyia utafiti na kuifundisha katika sehemu mbalimbali kama vile shuleni na vijijini. Michezo ya jadi ina nafasi kubwa katika utamaduni wetu na inaweza kuendelezwa kwa urahisi kuliko michezo ya kigeni, kwani wataalamu wake wapo hapa hapa nchini. Ni imani yangu kwamba kutokana na dira hii wapenzi na viongozi wote wa michezo watashirikiana na wanamichezo kuweka msukumo mpya katika michezo yote.

**Sera** hii ni matokeo ya juhudi za pamoja za mawazo ya wote wanaohusika na utekelezaji wa maendeleo ya michezo. Matayarisho ya **Sera** hii yalianza 1985. Kwa sababu ya historia ndefu ya matayarisho ya **Sera** hii ni dhahiri kuwa imepata mchango mkubwa wa mawazo na kuchambuliwa vya kutosha. Napenda kuwashukuru wote waliochangia ingawa ni vigumu kuwataja wote. Natoa shukrani zangu kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais ilikokuwa Sekta ya Utamaduni mwaka

1985 na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya matayarisho ya toleo la kwanza la rasimu ya **Sera** hii marehemu Wilfred Mwabulambo. Wengine ambao napenda kuwashukuru kwa michango yao ni viongozi wa Wizara iliyokuwa ya Maendeleo ya Jamii, Utamaduni, Vijana na Michezo, Jumuiya ya Wanawake na Jumuiya ya Vijana, Baraza la Michezo la Taifa, Idara za Utamaduni za Mikoa na Wilaya, Kamati ya Olimpiki ya Tanzania, Vyama vya Michezo vya Taifa, waandishi wa habari za michezo na wapenzi wote wa michezo. Mwisho, napenda niwashukuru wote walioshiriki katika kuandika, kuchapa, kujalidi na kukamilisha **Sera ya Maendeleo ya Michezo** Tanzania.

Prof. Philemon M. Sarungi (MP)
WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI

Dar es Salaam
Juni 1995

# SERA YA MAENDELEO YA MICHEZO

## 1. UTANGULIZI;

Michezo ni sehemu muhimu sana katika utamaduni wa kila jamii ya binadamu duniani kote. Kila kipindi cha historia ya binadamu kinaonyesha jinsi binadamu alivyobuni na kuendeleza michezo kulingana na mazingira yake ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kutokana na mabadiliko ya mazingira hayo michezo iliyochezwa na jamii ilikuwa inabadilika mara kwa mara. Baadhi ya mabadiliko hayo ni pamoja na hali ya mchezo, sheria na kanuni ili kukidhi mabadiliko hayo.

Tanzania kama jamii tulikuwa tukishiriki katika michezo mbalimbali katika kabila zetu. Tulishiriki katika michezo ya mieleka, kutupa mkuki, kulenga shabaha kwa upinde na mishale, sarakasi, kukimbia, kuruka, kuogelea, kucheza bao n.k.

Madhumuni ya michezo hii yalikuwa ni:-

(i) Kutoa burudani kwa jamii baada ya kazi;
(ii) Kujenga na kukomaza afya ya mwili na akili;
(iii) Kujenga ukakamavu, nidhamu na uwezo wa kujihami kwa mtu binafsi na kwa jamii.
(iv) Kuonyesha uwezo na vipaji vya washiriki na kutangaza hulka ya jamii kwa jaminyingine;
(v) Kuwa kiungo baina ya jamii mbalimbali;
(vi) Kukuza na kuendeleza uhusiano wa kirafiki baina ya jamii mbalimbali.

Katika mazingira ya kikabila kama yalivyokuwa katika jamii zetu nyingi, Kanuni za mfumo wa kikabila zilitawala uendeshaji wa shughuli za michezo.

Kuingia kwa wageni na wakoloni nchini mwetu kuliambatana na kuingizwa kwa michezo ya kigeni kama Mpira wa Miguu, Hoki, Netiboli, Ndondi, n.k. Mchezo wa Riadha ambao ulikuwa ukichezwa katika jamii zetu nyingi kabla ya ujio wa wageni hawa, ulileta katika sura mpya ya kisasa na inayotambulika Kimataifa. Kadri nchi yetu ilivyozidi kuingia katika ulingo wa Kimataifa ndivyo michezo mingi zaidi ilivyoingia nchini na kuimarika. Michezo kama Mpira wa Miguu, Mpira wa Kikapu, Mpira wa Wavu, Tennis, Mpira wa Meza, Mpira wa Mikono, Kriketi, Golf, Baiskeli na kadhalika, kila mmoja uliweza kujipatia umaarufu kulingana na wakati.

Pamoja na kwamba michezo ya kigeni ilisaidia sana kufanya nchi yetu ijiunge na ulimwengu wa michezo athari kubwa iliyopatikana ni kuifanya michezo yetu ya jadi kudharauliwa na kupuuzwa hata ikafifia, hivyo kutufanya kana kwamba hatukuwa na michezo yetu wenyewe.

**Mabadiliko baada ya kupata Uhuru (1961):**

(i) Mara baada ya kupata Uhuru, Serikali mpya ya Tanganyika ilitangaza nia yake ya kufufua, kuimarisha, kukuza na kuendeleza vielelezo vya utamaduni wetu, ikiwemo michezo. Mwaka 1962 Serikali iliunda Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana na kuikabidhi kazi na jukumu la kuendeleza michezo nchini pamoja na

kuiendesha kwa mfumo unaoeleweka zaidi na unaolingana na mahitaji, mwelekeo na matakwa ya Taifa.

(ii) Mwaka 1967 Bunge la Jamhuri ya ~Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheira Na. 12 iliyonzisha rasmi Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ambalo lilipewa jukumu la kuongoza na kuratibu maendeleo ya michezo kwa kushirikiana na Vyama vya Michezo vya Taifa.

(iii) Kuanzia mwaka 1969 Michezo iliundiwa Idara maalum chini ya Sekta ya Utamaduni ambayo mwaka huo Wizara ya Utamaduni iliunganishwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni.

(iv) Mwaka 1973 katika Mkutano Mkuu wa 16 wa Chama Tawala cha TANU lilipitishwa Azimio lililotaka michezo ipewe kipaumbele na ionekane kuwa ni sekta muhimu katika uhai wa Taifa letu.

(v) Kuanzia mwaka 1971 Vyama vya Michezo vilivyokuwapo viliundwa upya na vingine vingi vikaundwa, ili kuwa na mfumo mzuri wa kuliwezesha Baraza kusimamia shughuli za Vyama hivyo.

(vi) Mwaka 1974 Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana iliundwa tena na ikapewa jukumu ła kufufua, kuimarisha, kuendeleza na kusimamia michezo nchini.

(vii) Mwaka 1980 sekta ya Utamaduni iliunganishwa na Sekta ya Habari kuunda Wizara ya Habari na Utamaduni.

(viii) Mwaka 1984 Sekta ya Utamaduni ilihamishiwa katika ofisi ya Waziri Mkuu.

(ix) Mwaka 1985 iliundwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Utamaduni, Vijana na Michezo.

(x) Mwaka 1990 Sekta ya Utamaduni ilihamishiwa tena katika Wizara ya Elimu na ikaundwa Wizara ya Elimu na Utamaduni.

**Hali ya sasa:**

Tangu kuanzishwa kwa Wizara yenye dhamana ya michezo na Baraza la Michezo la Taifa, maendeleo katika maeneo mbalimbali ya michezo yamepatikana.

(a) Baadhi ya wachezaji wetu wameshiriki kwa mafanikio makubwa katika michezo ya Kimataifa na kusaidia kulitangaza Taifa letu nje ya mipaka yake.

(b) Michezo mingi mipya imeanzishwa na kuenezwa nchini kwa madhumuni ya kuwapatia Watanzania wengi nafasi ya kushiriki kulingana na vipaji na uwezo na mapenzi yao. Aidha wananchi wengi zaidi wametambua umuhimu wa michezo.

(c) Baadhi ya Wizara, Idara, Mashirika ya Umma, Makampuni na Taasisi mbalimbli, kwa kutambua umuhimu wa michezo zimeanzisha shughuli za michezo kwawafanyakazi wao katika sehemu zao za kazi.

(d) Ili kuwasaidia wananchi kupenda na kushiriki zaidi katika michezo, nchi marafiki za Sweden, Norway, Finland na Denmark zimegharamia Miradi ya Michezo kwa Wote katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mtwara na Mwanza. Miradi hiyo imesaidia katika kuwelimisha wananchi juu ya manufaa na umuhimu wa Michezo kwa afya zao.

(e) Hatua nyingine muhimu zilizochukuliwa katika kuleta maendeleo katika michezo ni pamoja na:

(i) Ujenzi wa viwanja vya kisasa katika maeneo mbalimbali.

(ii) Ufudishaji wa taaluma za michezo kama ualimu, utawala na uamuzi wa michezo.

(iii) Uanzishaji wa mafunzo ya juu katika taaluma za michezo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

(iv) Maandalizi ya wataalam wa michezo katika nyanja mbalimbali yamefanyika kutokana na misaada ya nchi marafiki.

**Matatizo yaliyojitokeza:-**

Pamoja na mafanikio na dalili za maendeleo ya michezo zilizotajwa hapo juu, yapo matatizo yanayopunguza kasi ya maendeleo hayo. Baadhi ya matatizo hayo ni:-

(i) Uhaba mkubwa wa vyuo vya taaluma ya michezo na upungufu wa wataalam wa michezo;

(ii) Kutofundishwa kwa somo la Elimu kwa Michezo shulen na vyuoni;

(iii) Utunzaji na usimamizi mbaya wa viwanja vya michezo vilivyopo;

(iv) Uvamizi wa viwanja vya michezo na burudani kwa watoto;

(v) Upungufu mkubwa wa viwanja vyenye hadhi ya Kimataifa;

(vi) Ukosefu wa viwanda vya kutengenezea vifaa vya michezo nchini na gharama kubwa ya vifaa hivyo vitokavyo nchi za nje;

(vii) Kuhamahama kwa Idara ya Michezo toka Wizara hadi Wizara;

(viii) Ufinyu wa bajeti ya kuendeleza michezo;

(ix) Kutokuwepo na desturi ya wananchi kucheza michezo kwa ajili ya afya zao;

(x) Kushindwa kuwatumia kikamilifu wataalam wachache waliopo nchini;

(xi) Kutojua kwa Taasisi pamoja na vyombo mbalimbali na makundi yanayoshughulikia michezo au kushindwa kwao kutekeleza wajibu wao wa kuendeleza michezo katika sehemu zao;

(xii) Kutokuwa na Sera na mipango mizuri yakitaifa ya kuendesha michezo;

(xiii) Kutokuwa na muundo na utaratibu wa utawala mzuri wa kuendesha michezo.

## 2.0. Umuhimu wa Michezo katika Jamii:

Michezo ikiwa ni kiungo muhimu cha utamaduni katika jamii yetu, umuhimu wake ni kama ifuatavyo:-

(i) Kujenga na kuimarisha afya njema na maisha bora kwa wote;

(ii) Kujenga tabia ya ushirikiano, upendo, udugu na uzalendo;

(iii) Kujenga Taifa lenye nidhamu;

(iv) Kujenga uhusiano, uelewano na mshikamano wa Taifa;

(v) Kujenga moyo wa kishujaa na kujihami kukuza ukakamavu ujasiri na kujiamini;

(vi) Kuwapatia wananchi burudani;

(vii) Kulitambulisha na kulitangaza Taifa nje ya mipaka yake;

(viii) Kumjenga mchezaji kuwa mtu kamili - kimwili, kiakili na kiroho kuanzia utotoni hadi uzeeni.

## 2.1 MADHUMUNI YA SERA

Ili kuweza kulikwamua Taifa letu katika janga hili la kukosa maendeleo ya kimichezo kwa ajili ya afya bora ya wananchi, sifa na heshima ya Taifa, Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya michezo imetambua na kuamua kwamba mbinu pekee ya kutatua matatizo yaliyopo na kuleta mafanikio na maendeleo ya kudumu katika michezo ni kuwa na SERA ambayo itatoa malengona mipango ya taifa,, maelekezo na miongozo ya jumla kuhusu uendeshaji wa michezo katika Taifa. Madhumuni ya SERA hii ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa ufafanuzi juu ya umuhimu wa michezo katika jamii;

(ii) Kuweka malengo na mipango ya kuendeleza michezo;

(iii) Kufafanua majukumu na kutoa mwongozo kwa vyombo mbalimbali vya michezo kama vile Baraza la Michezo la Taifa, vyama vya michezo n.k.;

(iv) Kutoa mwongozo wa namna ya kushirikisha sekta nyingine ambazo umuhimu wake katika kufanikisha michezo hauwezi kuepukwa;

(v) Kushirikisha vyombo vya fedha pamoja na makampuni na watu binafsi (NGOs) katika kugharamia maendeleo ya michezo nchini;

(vi) Kubainisha muundo na utaratibu mzuri wa kusimamia maendeleo ya michezo nchini.

## 4.0 MALENGO NA MIPANGO YA MAENDELEO YA MICHEZO

Ili madhumuni yanayoorodheshwa katika Sera hii yaweze kufikiwa na faida za michezo katika jamii zipatikane ni muhimu yawekewe malengo na mipango ya utekelezaji. Malengo na mipango hiyo ni kama ifuatavyo:

(i) Uhamasishaji wa Umma wa Tanzania kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo;

(ii) Upatikanaji wa viwanja na zana bora na za kutosha kwa ajili ya kuimarisha maendeleo ya michezo;

(iii) Uandaaji na utayarishaji wa wataalam wa kutosha katika fani na taaluma mbali mbali za michezo;

(iv) Uhakikisho wa timu na wachezaji wetu kufanya vizuri katika mashindano na michezo ya kimataifa;

(v) Utafiti katika michezo ya jadi kwa lengo la kufufua na kuiendeleza.

(vi) Ushirikiano na mataifa mengine katika utoaji wa Elimu kwa Michezo na Michezo.

## 5.0 VYOMBO VYENYE JUKUMU LA KUTEKELEZA SERA YA MICHEZO:

Utekelezaji wa madhumuni ya michezo unahitaji ushirikiano wa hali ya juu miongoni mwa vyombo mbalimbali vinavyohusika n michezo katika kutoa huduma zinazohusika na kuhitajika katika kuendeleza michezo kwa ajili ya maendeleo ya jamii
**Vyombo hivyo ni:**

(i) Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya michez

(ii) Baraza la Michezo la Taifa;

(iii) Mabaraza ya Michezo ya Mikoa na Wilaya;

(iv) Vyama vya Michezo, Vilabu na Mashirikisho ya Michezo;

(v) Kamati ya Taifa ya Olimpiki (TOC).

(vi) Wizara mbalimbali, Idara za Serikali, Mashirika ya Umma na ya binafsi, Taasisi mbalimbali ikiw ni pamoja na Vyama vya kisiasa, vya wafanyaka na wakulima, na watu binafsi.

## 5.1 KAZI ZA VYOMBO HIVYO:

5.1.1. Wizara yenye dhamana ya michezo. Wizara hii inayo majukumu mallum katika kusimamia na kuendeleza michezo nchini. majukumu hayo ni:-

(a) Kuandaa mipango na mafunzo ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kupata wataalam wa michezo w

kutekeleza mipango iliyowekwa na pia kutumia vema wale waliopo;

(b) Kusimamia na kuratibu fedha za kugharamia mipango ya maendeleo ya michezo;

(c) Kusimamia Sera ya Michezo kuhusu upatikanaji, uendelezaji na utumiaji wa zana, nyenzo na vifaa vingine vya michezo. Umilikaji wa viwanja vya michezo na viwanda vya vifaa vya michezo vilivyopo nchini.

(d) Kuweka utaratibu wa uhusiano wa kimichezo kati ya Tanzania na nchi za nje ; kwa mfano mikataba ya ushirikiano n.k.;

(e) Kutoa ushauri wa kitaalam popote pale unapotakiwa katika harakati za kuendeleza michezo;

(f) Kuweka utaratibu wa uhusiano katika kuendeleza michezo baina ya Wizara za Serikali na vyombo vingine vya taifa;

(g) Kutoa maelekezo kwa Baraza la Michezo la Taifa kuhusu maendeleo ya michezo kama yalivyofafanuliwa katika sheria ya Baraza la Michezo la taifa;

(h) Kuweka mipango thabiti ya kuimarisha na kuendeleza Tiba kwa Wanamichezo;

(i) Kuweka mipango thabiti ya kuendeleza michezo kwa wote;

(j) Kuhakikisha kuwa kunakuwepo mafunzo kwa Wataalam wa Michezo na Wanamichezo nchini kwa kushirkiana na mashirika ya kitaifa na kimataifa taasisi mbalimbali na watu binafsi katika kuimarisha na kuendeleza Vyuo vya Michezo nchini hasa kwa kuanzia na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

**5.1.2 Wizara yenye dhamana ya Elimu. Majukumu yake ni:-**

(a) Kuandaa utaratibu wa kufundisha Elimu kwa Michezo na michezo kuanzia shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu hadi Chuo Kikuu;

(b) Kutekeleza kwa ukamilifu azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Elimu kwa Michezo na Michezo (Physucal Education Charter) la 1978 kwa kushirkiana na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa yanayojihusisha na michezo na utamaduni kama vile Tume ya Taifa ya Sayansi Elimu na Utamaduni, UNESCO;

(c) Kuhakikisha kwamba walimu wa kufundisha somo la Elimu kwa Michezo na Michezo katika Shule na Vyuo wanaandaliwa vya kutosha;

(d) Kuhakikisha kwamba mashindano ya michezo yanayoendeshwa katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu yanaimarishwa ili

yaendelee kuchangia upatikanaji wa wachezaji bora wa taifa, pia wenye uwezo wa kuendeleza taaluma ya michezo;

(e) Kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya Michezo kutayarisha mitaala pamoja na kuandika vitabu ambavyo vitatumika kufundisha Elimu kwa Michezo na Michezo shuleni na vyuoni kwa misingi ya kuoanisha mafunzo haya na yatakayotolewa na Vyama vya Michezo nje ya taasisi hizo ili kuweka msingi imara wa michezo.

(f) Kuhakikisha kwamba viwanja vya michezo vya shule na vyuo vinaendelea kutunzwa na kutumika kwa madhumuni ya shughuli za michezo;

(g) Kufuatilia utekelezaji wa mitaala na mipango yote ya michezo shuleni na vyuoni.

### 5.1.3 Baraza la Michezo la Taifa

Kazi za Baraza la Michezo la Taifa zimeelezwa wazi wazi katika Sheria ya Bunge Na. 12 ya 1967 pamoja na Marekebisho yake katika sheria Na. 6 ya 1971.

Jukumu kubwa la Baraza ni kuendeleza michezo nchini kwa kushirikiana na Vyama vya Michezo. Kwa mujibu huo kazi muhimu za Baraza ni:

(a) Kuvisaidia na kuvielekeza Vyama vya Michezo kwa kuandaa mafunzo kwa viongozi wa vyama na Vilabu vya Michezo;

(b) Kutoa maelekezo kwa vya vyama vya michezo juu ya ujenzi wa viwanja vya michezo;

(c) Kutafuta vifaa vya Michezo na kuvisambaza kwa wanaovihitaji;

(d) Kuandaa utaratibu wa kujenga uhusiano wa kimichezo kati ya Vyama vya Michezo na wachezaji wenyewe;

(e) Kuchambua na kuthibitisha ratiba za mashindano ya Michezo zinazoandaliwa na Vyama vya Michezo vya taifa

(f) Kuandaa tamasha la Michezo kitaifa kwa kushirikiana na vyama vya michezo;

(g) Kuishauri Wizara juu ya uhusiano wa kimichezo na mataifa mengine.

(h) Kuandaa na kutekeleza mbinu mbalimbali za kusisimua mwamko wa michezo kwa jumla, kama vile kutengeneza na kutoa medali za michezo, kutoa misaada au nafasi za mafunzo ya michezo (Scholarships), kuendesha zahanati za michezo, n.k.

(i) Kuhakikisha kuwa fedha za Vyama na Vilabu vya Michezo zinakaguliwa na matumizi mabaya ya fedha yanaondolewa katika Vyama hivyo.

### 5.1.4 Mabaraza ya Michezo ya Mikoa na Wilaya:

Kazi za Mabaraza haya zimeelezwa katika Tangazo la Serikali Na.471 tarehe 16 Novemba, 1990. Shughuli za Mabaraza hayo zitakuwa kama hizo zilizoorodheshwa chini ya Baraza la Michezo la Taifa (5.1.2 (a)-(i)) kwa utendaji wa ngazi inayohusika.

### 5.1.5 Vyama vya Michezo:

Hivi vimo katika makundi matatu makubwa.

(a) Vyama vya ridhaa vilivyosajiliwa na Msajili wa vyama vya michezo na kujishirikisha na Baraza la Michezo la Taifa;

(b) Mashirikisho ya Michezo ambayo yameundwa na taasisi mbalimbali ili kutoa burudani za kimichezo kwa wafanyakazi, kuwakutanisha wachezaji wao ili wafahamiane, pia kuwashindanisha katika michezo inayohusika na kupata mabingwa wao katika ngazi ya Taifa;

(c) Vyama vya michezo ya kulipwa ambavyo vimesajiliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani,

Wajibu mkubwa wa chama cha mchezo ni kuwaunganisha wanamichezo unaohusika Kitaifa na kusimamia maendeleo ya mchezo huo. Kazi muhimu za vyama vya michezo:-

(a) Kuandaa Katiba sahihi za kuwaunganisha wanachama zinazoonyesha waziwazi madhumuni ya Chama kinachohusika, misingi ya upatikanaji fedha, taratibu za uchaguzi wa viongozi, kazi zitakazofanywa kwa kipindi fulani, n.k;

(b) Kuandaa mashindano ya kuendeleza michezo ndani na n ya nchi;

(c) Kuweka kumbukumbu za maendeleo ya wachezaji wake bora;

(d) Kupata vifaa vya kuendeleza michezo na kujenga viwanj vya michezo kwa kushirikiana na Baraza la Michezo la Taifa na vyombo vingine vya michezo.

(e) Kuweka utaratibu wa kuendesha mashindano mpaka; vijijini;

(f) Kutunza hesabu za fedha na kutoa taarifa yake kwa Baraza la Michezo kila mwaka;

(g) Kulinda na kusimamia nidhamu ya vilabu, wanachama na viongozi mbali mbali.

### 5.1.6 Vilabu vya Michezo:

Wajibu wa Vilabu vilivyo sajaliwa na msajili wa Vyama vya Michezo utakuwa kama ulivyowekwa katika Katiba zake. Hatahivyo wajibu mkubwa wa kila Kilabu ni kulea wachezaji wake na kuendeleza mchezo au michezo iliyokubalika kikatiba.

### 5.1.7 Kamati ya Taifa ya Olimpiki (TOC):

Kamati hii inawakilisha Tanzania katika Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki. Wanachama wake wakuu ni Vyama vya taifa vya Michezo inayochezwa katika Olimpiki na katika michezo ya Jumuiya ya Madola. Kwa mujibu wa Sheria na maelekezo ya Kamati ya Kimataifa ya Olimpiki, kazi kubwa ya Kamati ya Taifa ni kufanya maandalizi ya timu za mashindano ya Kimataifa. Hata hivyo kwa mujibu wa taratibu zetu za uongozi wa michezo, Kamati hii inadhibitiwa na Baraza la Michezo la Taifa. Kwa hiyo:-

(i) Itashirikiana na Vyama vya Michezo, Baraza la Michezo la Taifa na Wizara yenye dhamana ya michezo kuandaa timu zinazoshiriki katika mashindano ya Kimataifa na kuhakikisha kwamba maandalizi yanafanywa ili kuliletea Taifa ushindi;

(ii) Ikishirikiana na Vyama vya Michezo, Baraza la Michezo la Taifa na Wizara yenye dhamana ya michezo na vyombo vingine vinavyojihusisha na michezo Kamati ya Olimpiki itaendeleza mafunzo, maadili na malezi mema ya Olimpiki kwa vijana.

## 5.1.8 WIZARA MBALIMBALI, IDARA ZA SERIKALI, MASHIRIKA YA UMMA, MAKAMPUNI, NA WATU BINAFSI:

(a) Wizara zenye majeshi. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani.

(i) Wakati wa amani majeshi yanayo nafasi nzuri ya kuwashirikisha vijana wake katika michezo ili kujenga afya zao, kuwaleta pamoja na kuwawezesha kufahamiana. Aidha kwa kuwa askari ni vijana wanao uwezo mkubwa wa kuliwakilisha Taifa katika michezo na mashindano ya Kimataifa. Kwa hiyo juhudi za kuendesha michezo katika vikosi na kuvishindanisha hadi ngazi ya Taifa zizidi kuimarishwa na kuendelezwa;

(ii) Wizara zenye majeshi zitaendelea kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya michezo pamoja na vyama vya Michezo kuweka taratibu ambazo zitayawezesha majeshi kutoa wawakilishi wengi kitaifa. Taratibu hizo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa walimu na waamuzi, wa michezo mbalimbali, kupata vifaa vya kutosha vya kufundishia michezo na kushindana na kutengeneza viwanja vinavyofaa kwa mashindano;

(iii) Majeshi pia yanayo jukumu la kueneza na kukuza michezo kwa wote ndani ya majeshi yenyewe kwa kuwa na utaratibu unaotekelezeka na kuwashirikisha askari wenye umri mkubwa katika michezo na mazoezi ya mwili. Kwa hiyo michezo ya ndani itabidi ipewe umuhimu maalum kwa kujengewa viwanja pamoja na kupatiwa vifaa vinavyohitajika;

(iv) Idara ya Uhamiaji itadhibiti uingiaji nchini wa wachezaji na walimu wanaoweka mikataba na vilabu bila kufuata taratibu za nchi.

(b) **WIZARA YA TAWALA ZA MIKOA, NA SERIKALI ZA MITAA**

(i) Ofisi za Mikoa na Wilaya za Wizara hii zinao wajibu wa :- Kutoa maelekezo kwa Mabaraza ya Michezo kwa ngazi zinazohusika kuhusu muundo, sera ya kuendeleza michezo na majukumu mengine kama yanavyotajwa katika Kanuni za Baraza la Michezo kwa ngazi inayohusika;

(ii) Kuunganisha shughuli za Vyama vya Michezo kwa kuandaa mashindano ya michezo ya vyama hivyo katika sherehe za tamasha za kimkoa na wilaya;

(iii) Kuratibu shughuli za vyama vya michezo Mikoani, Wilayani na katika Halmashauri za Miji, kwa kuwapa ushauri juu ya Sera, mafunzo na misingi ya kupata fedha za kuendeleza michezo;

(iv) Kushirikiana na viwanda na mashirika yaliyomo mkoani kuandaa utaratibu wa kueneza michezo kwa wote viwandani na katika maeneo yanayozunguka;

(v) Kuandaa mpango wa mkoa, wilaya au mji wa muda mfupi na mrefu na kuweka taratibu za utekelezaji kwa ajili ya kuleta maendeleo katika michezo;

(vi) Kujenga viwanja vya michezo na maeneo ya burudani;

(vii) Kuthibiti na kuhakiki matumizi halali ya maendeo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo na burudani.

c) **WIZARA YA KAZI NA MAENDELEO YA VIJANA**

(i) Kushirikisha vijana katika michezo;

(ii) Kuandaa sehemu za burudani kwa vijana

(iii) Kuhimiza Idara ya Ustawi wa Jamii kuanzisha vikundi vya michezo kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum ;

(iii) Majeshi pia yanayo jukumu la kueneza na kukuza michezo kwa wote ndani ya majeshi yenyewe kwa kuwa na utaratibu unaotekelezeka na kuwashirikisha askari wenye umri mkubwa katika michezo na mazoezi ya mwili. Kwa hiyo michezo ya ndani itabidi ipewe umuhimu maalum kwa kujengewa viwanja pamoja na kupatiwa vifaa vinavyohitajika;

(iv) Idara ya Uhamiaji itadhibiti uingiaji nchini wa wachezaji na walimu wanaoweka mikataba na vilabu bila kufuata taratibu za nchi.

(b) **WIZARA YA TAWALA ZA MIKOA, NA SERIKALI ZA MITAA**

(i) Ofisi za Mikoa na Wilaya za Wizara hii zinao wajibu wa :- Kutoa maelekezo kwa Mabaraza ya Michezo kwa ngazi zinazohusika kuhusu muundo, sera ya kuendeleza michezo na majukumu mengine kama yanavyotajwa katika Kanuni za Baraza la Michezo kwa ngazi inayohusika;

(ii) Kuunganisha shughuli za Vyama vya Michezo kwa kuandaa mashindano ya michezo ya vyama hivyo katika sherehe za tamasha za kimkoa na wilaya;

(iii) Kuratibu shughuli za vyama vya michezo Mikoani, Wilayani na katika Halmashauri za Miji, kwa kuwapa ushauri juu ya Sera, mafunzo na misingi ya kupata fedha za kuendeleza michezo;

(iv) Kushirikiana na viwanda na mashirika yaliyomo mkoani kuandaa utaratibu wa kueneza michezo kwa wote viwandani na katika maeneo yanayozunguka;

(v) Kuandaa mpango wa mkoa, wilaya au mji wa muda mfupi na mrefu na kuweka taratibu za utekelezaji kwa ajili ya kuleta maendeleo katika michezo;

(vi) Kujenga viwanja vya michezo na maeneo ya burudani;

(vii) Kuthibiti na kuhakiki matumizi halali ya maendeo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo na burudani.

## c) WIZARA YA KAZI NA MAENDELEO YA VIJANA

(i) Kushirikisha vijana katika michezo;

(ii) Kuandaa sehemu za burudani kwa vijana

(iii) Kuhimiza Idara ya Ustawi wa Jamii kuanzisha vikundi vya michezo kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum ;

(iv) Kuhamasisha vijana wote katika kushiriki michezo.

(d) **WIZARA YA AFYA**

Ihamasike na kuandaa utaratibu wa kuimarisha huduma ya tiba ya Wanamichezo:-

(i) Kuweka vifaa vya uchunguzi vya kimichezo na wataalam katika hospitali za rufaa ili kuweza kufanya utafiti mbalimbali;

(ii) Kuweka kliniki za michezo katika kila uwanja mkubwa wa michezo;

(ii) Kuanzisha somo la tiba ya wanamichezo katika vyuo vya tiba nchini.

(e) **WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

Hii ina jukumu la kuhamasisha na kushawishi wenye viwanda na wawekezaji vitega uchumi:

(i) Kutengeneza vifaa vya michezo ili kupunguza gharama za kuviagiza nje;

(ii) Kushawishi wenye uwezo kuagiza vifaa vya michecho na kuanzisha maduka ya vifaa hivyo;

(iii) Maendeleo ya michezo nchini itafanywa kuwa ni eneo la uwekezaji wa raslimali katika sera ya kuhimiza uwekezaji wa raslimali (Investiment Promotion Policy).

(f) **WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO MIJINI:-**

(i) Itaendelea kutenga maeneo ya kujenga viwanja vya michezo na vya burudani katika miji, vijiji, shule, vyuo, viwanda na taasisi nyinginezo;

(ii) Itahakikisha kwamba viwanja vya michezo na maeneo ya burudani popote yalipo yanalindwa na kutumiwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa;

(iii) Itahakikisha kuwa wenye viwanja vya michezo mijini na vijijini wanapewa hati miliki.

(g) **WIZARA YA MALIASILI, UTALII NA MAZINGIRA:-**

Kwa kuwa michezo inayo nafasi kubwa ya kuleta watalii nchini, Wizara hii itashirikikatika kuiendeleza michezo kwa:-

(i) Kuanzisha utaratibu wa kuwa na viwanja vya michezo katika mahoteli, mbuga za wanyama na vituo vingine vya kitalii;

(ii) Kuzitumia timu zetu za michezo kutangaza maeneo ya utalii nchini watokapo nchini kwenda kucheza nchi za nje.

h) **WIZARA NYINGINE, IDARA ZA SERIKALI, MASHIRIKA YA UMMA, MAKAMPUNI NA WATU BINAFSI**

(i) Wote watawajibika kutoa nafasi kwa wafanyakazi kushiriki katika michezo;

(ii) Kila Wizara, Idara ya Serikali, Shirika, Kampuni na Watu Binafsi, watakuwa na wataalam wa michezo katika sehemu zao za kazi au maeneo wanakoishi ili wafundishe michezo katika taasisi zao;

(iii) Kila Wizara, Idara, Shirika, Kampuni na Watu binafsi, watakuwa na mipango kamili ya kuendesha michezo;

(iv) Mashirika na Makampuni yatakuwa mstari wa mbele katika kutoa michango ya hali na mali kwa ajili ya maendeleo ya michezo nchini;

(v) Wizara, Idara, Mashirika na Makampuni, yatawaendeleza wafanyakazi wao wenye vipaji vya michezo kwa kuwachezesha katika timu za mahali pa kazi na kuwaruhusu kushiriki katika mashindano mengine.

## 5.2 UCHAGUZI WA VIONGOZI WA MICHEZO:

Kwa mujibu wa taratibu zilizopo, vyombo vyote vya michezo vinaongozwa na kutawaliwa na Sheria na Katiba zilizopo. Mfumo wa uongozi na utawala ulilopo sasa katika ngazi ya Taifa, Mikoa na Wilaya, utaendelezwa hadi ngazi ya Vijiji kwa madhumuni ya usimamizi mzuri wa michezo katika ngazi zote.

5.2.1 Baraza la Michezo la Taifa likishirikiana na vyama na Vilabu vya Michezo litaandaa utaratibu mzuri na kuweka Kanuni thabiti kuhusu usimamizi wa fedha, utunzaji wa mali za vyama, Vilabu na vyombo vingine inavyohusika na michezo.

5.2.2 Wizara yenye dhamana ya michezo na Baraza la Michezo la Taifa kwa kupitia vyama vya Michezo, watahakikisha kuwa watu wanaopewa dhamana ya uongozi wa michezo ni watu walio na sifa zinazokubalika.

Kwa mujibu huo kiongozi wa michezo atatakiwa awe na sifa zifuatazo:-

(i) Awe na utaaalam wa michezo anaotaka kuongoza;
(ii) Awe na uzoefu wa kuongoza pia na taaluma za uongozi wa michezo;
(iii) Awe na nidhamu inayokubalika;
(iv) Awe ni raia wa Tanzania.
(v) Awe mzalendo na mwenye kupenda michezo;
(vi) Awe mwaminifu, mpenda haki na mkweli.

Vyombo vinavyohusika na usimamizi wa uchaguzi kwa kila ngazi vitatayarisha utaratibu unaofaa wa jinsi ya kuwapata viongozi wenye sifa zinazotakiwa.

5.2.3 Kwa ajili ya kuepusha umilikaji wa muda mrefu wa vyombo vya michezo na wanaochaguliwa kuviongoza, uwe utaratibu wa kila chombo cha michezo kwamba viongozi wake wa juu (Mwenyekiti), Katibu na Mweka Hazina) wataruhusiwa kugombea nafasi hizo kwa vipindi vitatu vya miaka mitatu kila kipindi, isipokuwa Kamati ya Olimpiki (TOC). Viongozi wake watagombea kwa vipindi viwili vya miaka minne kila kipindi.

Baada ya muda huo kiongozi anaweza tu kuwa mjumbe wa kushirikishwa.

## 6. UTARATIBU NA UENDESHAJI WA MICHEZO MBALIMBALI

Maeneo na makundi yafuatayo ndiyo yatakayozingatiwa katika utaratibu na uendeshaji wa michezo:-

(i) Michezo ya Jadi;
(ii) Michezo kwa Wote;
(iii) Michezo ya Mashindano;
(iv) Michezo kwa ajili ya vikundi vyenye mahitaji maalum;
(v) Michezo na mazoezi ya viungo kwa wanawake.
(vi) Michezo ya kulipwa.

### 6.1 Michezo ya Jadi:

Hii ndiyo itakayoendelea kuonyesha na kudhihirisha kwa vizazi vyetu vijavyo na kwa wageni kwamba Utamaduni wetu wa asili ulijumuisha michezo. Ili kuifufua, kuieneza na kuiendeleza michezo hiyo itabidi:-

(a) Ifanyiwe utafiti kuhusu aina yake, sheria na kanuni za kuiendesha.
(b) Ifundishwe Vijijini na Mijini na hasa shuleni kulingana na mazingira;
(c) Iandaliwe wataalam wa kuiendesha katika ngazi zote, aidha iandaliwe vifaa pamoja na viwanja;

(d) Iandaliwe mashindano kuanzia ngazi ya kijiji hadi Kitaifa kwa ajili ya kupata mabingwa wake.

## 6.2 Michezo kwa Wote:

Haki ya kila binadamu kupata fursa ya kufanya mazoezi ya viungo na kucheza imetamkwa katika mwongozo wa Kimataifa kuhusu Elimu kwa Michezo uliopitishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa na Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), mwaka 1978. Kwa kuwa lengo la Michezo ni kumjenga mtu mwenye afya bora, mwenye hamasa ya kutenda, mwenye msukumo wa kazi na aliyejengeka kimwili na kiakili, umma wote wa Tanzania hauna budi kushiriki kikamilifu katika michezo na mazoezi ya viungo.

Kama alivyowahi kusema Rais wa Kwanza wa Tanzania alipokuwa akifunga michezo ya Majeshi mwaka 1978, "Mazoezi ya mwili ni jambo la lazima kama kupumua. Watoto, Vijana wetu na watu wazima, lazima wajenge tabia ya kufanya mazoezi ya mwili. Mazoezi ya mwili humwezesha mtu viungo vyake kufanya kazi vizuri. Michezo itumike kujenga miili imara na akili safi."

Ili kuweza kufikia shabaha ya kueneza michezo kwa wote itabidi:-

(a) Serikali kwa kutumia vyombo mbalimbali kama vile radio, televisheni, magazeti, n.k., itaelimisha kikamilifu umma wote wa Tanzania juu ya umuhimu na faida za

kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo kwa manufaa yao;

(b) Serikali kwa kutumia Wizara zake - Wizara yenye dhamana ya Michezo; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Mijini; Wizara yenye dhamana ya Elimu; Wizara ya Utalii, Maliasili na Mazingira; Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana; Wizara ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa; zitawajibika kutenga na kuhifadhi maeneo ya viwanja vya michezo na burudani popote pale penye maskani ya watu na katika shule;

(c) Wizara yenye dhamana ya michezo kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda na Sekta ya binafsi, watahakikishe kuwa viwanda vya kutengeneza vifaa vya michezo nchini vinaimarishwa ili kupunguza uhaba wa vifaa hivyo;

(d) Vifaa vya michezo vya aina mbalimbali vinavyoagizwa kutoka nje kwa madhumuni ya michezo vitozwe kodi nafuu;

(e) Wizara yenye dhamana ya Elimu itaandaa na kutekeleza mikakati ya kufundisha elimu kwa michezo na michezo katika ngazi zote za elimu (shule za msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu) kwa kumwezesha kila mwananchi kujenga tabia ya kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo akiwa na elimu na stadi za kumwezesha kushiriki;

(f) Wizara yenye dhamana ya Michezo itashauri, itahimiza na itasimamia uendeshaji wa michezo ya jadi kama kichocheo cha kushiriki katika michezo kwa wote;

(g) Vikundi vya sanaa vilivyoko Mijini na Vijijini vitatumika kuwahamasisha wananchi kushiriki katika michezo.

## 6.3 Michezo ya Mashindano:

Hii ni michezo ya timu au ya mchezaji mmoja mmoja inayochezwa popote duniani kirafiki au kimashindano, ikitawaliwa na sheria za Kimataifa. Ili kuweza kupata ushindi katika mashindano ya aina hii, ujuzi na uwezo wa hali ya juu kwa kila mchezaji huhitajika. Kwa hiyo wanamichezo wanaochaguliwa kuwakilisha Taifa katika mashindano ya Kimataifa itabidi wawe wamefikia viwango vya Kitaifa na Kimatifa.

Ili tuweze kupata wachezaji bora wa kutuwakilisha, yafuatayo lazima yazingatiwe:-

(a) Ufundishaji wa michezo uimarishwe katika shule tunakoweza kuwapata kwa wingi wanamichezo chipukizi wenye vipaji ambao wataendeleza na hatimaye kuwa mabingwa wa Taifa. Kwa hiyo elimu kwa michezo iwe ni sehemu muhimu ya masomo kwa wanafunzi wote shuleni;

(b) Utaratibu wa mashindano utakaoshirikisha wachezaji wengi utaandaliwa katika ngazi zote - Mikoa, Wilaya,

Vijiji - Mashindano ya uchaguzi wa wachezaji walio bora yaanzie katika ngazi ya Vijiji, yahusishe, shule, vyuo, majeshi, timu za Mashirika ya Umma, Makampuni na vilabu vya watu binafsi. Aidha uwepo mfumo wa kushindanisha mabingwa wa makundi mbalimbali ili kupatikana na wachezaji bora kwa ajili ya mashindano ya kiwango cha juu zaidi;

(c) Wizara yenye dhamana ya michezo itashirikiana na Wizara nyingine pamoja na taasisi zinazojihusisha na michezo kuanzisha mafunzo, vituo vya tiba na vyuo vya michezo vitakavyowaandaa wachezaji na wataalam wengi na wenye ujuzi katika fani mbalimbali za michezo;

(d) Huduma za michezo kama vile vifaa na viwanja vya michezo na tiba kwa wanamichezo zitaanzishwa na zitaendelezwa katika ngazi zote. Aidha wawakilishi wa Taifa watapewa motisha mbalimbali watakapokuwa katika kambi za maandalizi, kwa mfano malazi na chakula bora, bima na matibabu;

(e) Mabingwa wanakaochaguliwa kuwakilisha Taifa katika mashindano ya Kimataifa wataandaliwa kuzingatia maadili ya Taifa letu, ili wajue kuwa wao ni mabalozi wetu wakiwa katika mashindano hapa nchini au ugenini.

## 6.4 Michezo kwa Vikundi vyenye mahitaji maalum:

Faida za michezo ni muhimu pia kwa watu wenye mahitaji maalum kwa mfano:- walemavu, wasioona, viziwi, watu wenye taahira ya akili na aina nyingine za ulemavu. Mojawapo ya

malengo ya sera hii ni kutaka jamii na vyombo vinavyosimami michezo kuimarisha huduma za kimichezo kwa watu wenye mahitaji maalum kwa:-

(a) Kuwapatia vifaa vya michezo na viwanja;

(b) Kufunza wataalam wa michezo kwa walemavu na watu wenye taahira ya akili;

(c) Kuandaa mashindano maalum na kuwawezesha kushiri katika mashindano Kitaifa na Kimataifa;

(d) Kurekebisha sheria na Kanuni za michezo nchini ili zilingane na Sheria na Kanuni zinazotawala michezo kw watu wenye mahitaji maalum.

## 6.5 Michezo na mazoezi ya viungo kwa ajili ya Wanawake:

Kutokana na mila kongwe zinazokandamiza wanawake, wanawake wa Tanzania hawakuwa wakishiriki kikamilifu katik shughuli za michezo na mazoezi ya viungo. Hata wale waliobahatika kucheza katika ujana wao kabla ya kuolewa, hujikuta wanalazimika kujitoa katika michezo mara wanapoolewa. Athari kubwa ya tabia hii imekuwa ni kudhoofisha afya za akinamama wenyewe na kuwapunguzia uwezekano wa kuwahamasisha watoto wapende kucheza wang wachanga. Wizara yenye dhamana ya michezo kupitia Baraza l Michezo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Jumuiya ya Vijana n wanawake, zitafanya juhudi za makusudi za kuwahamasisha wanawake kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo ili

kujenga afya zao na kuwawezesha kuwalea watoto wa Tanzania kimichezo.

Juhudi zitakazofanyika ni:-

(a) Kuandaa na kufanya kampeni za kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa wanawake kushiriki katika michezo na kufanya mazoezi ya viungo;

(b) Kuanzisha vyama vya michezo na mazoezi ya viungo kwa ajili ya wanawake;

(c) Kutoa upendeleo wa makusudi kwa wanawake kushika nafasi za uongozi wa michezo aidha kupata nafasi za mafunzo na utaalam katika nyanja ya michezo.

(d) Kuelimisha jamii juu athari za baadhi ya mila na desturi katika ushiriki wa wanawake katika michezo na mazoezi ya viungo kwa ajili ya maendeleo yao.

## 6.6. MICHEZO YA KULIPWA

Hii ni michezo ambayo mchezaji hucheza kwa kulipwa chini ya mkataba maalum ambao hukubalika kati ya mmilikaji na mchezaji. Kutokana na hatu ambayo Tanzania imeshafikia katika baadhi ya michezo ya ridhaa hususan mpira wa miguu, na ili kuweka misingi thabiti katika uendelezaji wa vijapaji na maslahi ya wachezaji sera hii inaruhusu michezo ya kulipwa.

## 7.0 UJENZI NA UTUNZAJI WA VIWANJA VYA MICHEZO:

Huduma muhimu za kukuza na kuendeleza micheszo ni pamoja na ubora wa viwanja vya michezo. Kwa sababu hiyo:

(i) Serikali katika ngazi zake zote, kwa kushirikiana na wananchi itahakikisha kwamba vinakuwepo viwanja bora na vya kutosha na kumbi bora na za kutosha. Aidha yatatengwa maeneo maalum kwa ajili ya viwanja vya michezo na kumbi mbalimbali;

(ii) Kila taasisi yenye kiwanja au viwanja vya michezo itavitunza vizuri viwanja hivyo ili viweze kudumu,

(iii) Viwanja vikubwa (Stadium) vitatunzwa vizuri na vitakuwa chini ya uangalizi wa mameneja, wenye taaluma ya viwanja vya michezo;

(iv) Taasisi mbalimbali, mashirika na makampuni yatahimizwa kujenga viwanja vya michezo kwa ajili ya wafanyakazi wao;

(v) Kila Kilabu ya mchezo ihimizwe kuwa na uwanja wake wa michezo;

(vi) Watu binafsi wenye uwezo wapewe dhamana ya kujenga viwanja au kumbi zenye sifa za kitaifa na kimataifa, ili mradi michoro na vipimo vya viwanja/kumbi viwe vimeidhinishwa na Wizara yenye dhamana ya michezo;

(vii) Viwanja vyote vya michezo nchini vitapimwa na kupewa hati miliki;

(viii) Uvamizi wa viwanja vya michezo itakuwa ni kosa na sheria zitungwe kuwaadhibu wale wote

watakaovamia viwanja vilivyotengwa kwa ajili ya michezo katika ngazi zote; mijini mikoani wilaya na vijijini.

## 8.0. MAFUNZO KAMA MSINGI WA MAENDELEO YA MICHEZO

Ili michezo iendelee nchini mipango ya makusudi ya kuiendeleza lazima ifanywe:-

1 Somo la Elimu kwa Michezo liwe moja ya masomo ya msingi (coresubjects) katika shule na vyuo vya ualimu

2 Mafunzo yaanzie katika shule za msingi na yashirikishe wanafunzi wote ili:-

(i) Kumjenga kila mmoja kiafya ;

(ii) Kumjengea kila mmoja tabia ya kupenda kushiriki katika michezo na mazoezi ya viungo, ili baadaye aweze kushiriki vema katika michezo kwa wote;

(iii) Kumpatia kila mwanafunzi stadi za msingi za michezo mbalimbali zitakazomwezesha hapo baadaye kuchagua kwa uhakika mchezo anaoupendelea na kuumudu zaidi;

(iv) Kutumia fursa hiyo kutambua watoto wenye uwezo na vipaji maalum vya michezo ambao wataendelezwa ili wawe mabingwa wa Taifa wa baadaye.

(3) Wizara yenye dhamana ya Elimu itahakikisha kwamba:-

(i) Muhtasari wa mafundisho ya Elimu kwa Michezo ulioandaliwa kwa makusudi ya kujenga msingi

inayotakiwa katika shule za msingi na sekondari imechapishwa na kutolewa kwa shule zote na kutumiwa ipasavyo. Aidha somo la michezo litahiniwe katika ngazi zote;

(ii) Ualimu wa somo la elimu kwa Michezo ufundishwe katika Vyuo vyote vya Ualimu na kutahiniwa. Pia pawepo fursa kwa wanachuo wenye vipaji vya michezo kupewa mafunzo ya ziada (specialization) katika vyuo maalum vya michezo ili wakihitimu washughulikie watoto wenye vipaji vya michezo;

(iii) Mafunzo maalumu ya Ualimu wa Elimu kwa Michezo (Physical Education Certificate Course) yanayoendeshwa katika Chuo cha Ualimu Butimba yatolewe katika vyuo vingi zaidi kwa madhumuni ya kutoa walimu bora na wengi wa kuimarisha ufundishaji wa michezo katika shule za Sekondari na Vyuo. Aidha mafunzo ya ualimu wa elimu kwa michezo ngazi ya diploma yatolewe;

(iv) Wataalam wa Michezo wanaohitimu mafunzo yao katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Vyuo Vikuu vya nje watapata ajira zitakazohimiza matumizi ya Elimu waliyopata chuoni.

## 4.0 Mafunzo kwa Timu za Taifa:

Mafunzo kwa timu za Taifa yana kusudi kuwaleta pamoja wachezaji walioteuliwa kutoka katika makundi mbalimbali na kuwawezesha kucheza kama timu. Aidha yanakusudia :-

(i) Kumwandaa mchezaji kuwa katika hali ya kiwango cha juu (Top level performance) wakati wote;

(ii) Kuwezesha mchezaji kufikia lengo lake la kuwa nyota kamili ya Taifa;

(iii) Kuwaandaa wechezaji kimaaadili ili wawe na ari ya kuliwakilisha Taifa lao.

Ili kufanikisha madhumuni haya vyombo vinavyohusika na maandalizi ya timu vitaweka utaratibu wa kudumu wa kuifundisha timu kwa pamoja hivyo kupata muda wa kutosha wa kumshughulikia kila mchezaji binafsi kadri ya mahitaji yake. Utaratibu huo uwe na yafuatayo:-

(a) Programu ya mafunzo - hii ionyeshe:-

(i) Muda wa kukutanisha timu;

(ii) Mtiririko wa mafunzo;

(iii) Michezo ya majaribio.

Utaratibu wa mafunzo ya kudumu utamwezesha mwalimu wa timu ya Taifa kuwaelewa vizuri wachezaji wake na kugundua ubovu au uzuri wa timu yake ili afanye marekebisho yanayostahili. Pia katika muda huo mwalimu anaweza kuongeza au kupunguza wachezaji wanaostahili kuliwakilisha Taifa vizuri.

(b) Wakati wa maandalizi ya timu za Taifa kwa ajili ya mashindano ya Kimataifa, ihakikishwe kuwa utafiti wa awali wa mahali yatakapofanyika mashindano umefanywa na wataalam wanaohusika. Vivyo hivyo timu zetu ni sharti zifanyie mazoezi katika maeneo yenye mazingira yanayofanana na ya pale yatakapofanyika mashindano. Endapo mashindano yatafanyikia kwenye nchi au mji wenye joto, mazoezi nayo yafanyikie kwenye eneo lenye joto, kwa muda wa kutosha ili kuruhusu miili ya wachezaji kuwa inakubaliana na hali hiyo wakati wote wa mashindano.

## 9.0. UTEUZI WA TIMU YA TAIFA:

Nia ya serikali ni kuona kwamba kila mchezo unaochezwa hapa nchini unakuwa na timu ya taifa. Utaratibu wa uteuzi wao unaweza kutofautiana hapa na pale kufuatana na mazingira ya mchezo wenyewe. Hata hivyo mbinu zifuatazo zitumiwe:

(1) Mashindano ya Wilaya na Mikoa yaimarishwe na yatumiwe katika kuchagua wachezaji wa taifa. Pamoja na mashindano hayo mengine ya kitaifa kwa mfano Ligi za Taifa, mashindano ya Mashirika ya Umma, ya majeshi, ya Wizara na Idara za Serikali, ya shule, Vyuo na ya Kilabu Bingwa nayo yatumike katika kuchagua timu za taifa kwa michezo mbalimbali,

(2) Ili kufanikisha zoezi la uteuzi, vyombo vinavyohusika viunde kamati maalum za waataalamu ambazo zitapewa

madaraka ya kuchagua wachezaji wazuri kutokana na michezo mbalimbali.

(3) Uteuzi wa timu ya taifa utafanywa na kamati ya wataalam ya kitaifa ambayo itakuwa imeundwa na chama cha taaifa cha mchezo unaohusika. Uteuzi wa mwisho wa timu ya taifa utafanywa na mwalimu wa timu hiyo;

(4) Kila chama cha mchezo ambao unashindaniwa kitaifa na kimataifa lazima kiwe na timu mbili za kudumu ambazo ni timu za vijana na timu za wakubwa. Mtiririko huu lazima uanzie kwenye vilabu vya michezo mbalimbali, vyama vya wilaya, mikoa hadi ngazi ya taifa.

## 9.1 Malezi ya Wachezaji wa Timu ya Taifa:

Wachezaji wa taifa hata wale wa mikoa na wilaya hawana budi kuelewa nafasi waliyo nayo katika kuliletea taifa lao sifa na maendeleo kupitia katika michezo. Ili kufanikisha azma hii:-

(1) Serikali itahakikisha kwamba wachezaji wa taifa na ngazi nyingine wanaelewa maadili ya nchi na kucheza kwa kutetea taifa. Kwa hiyo kila chombo chenye wachezaji kifanye juhudi kuwapa malezi bora;

(2) Wizara yenye dhamana ya michezo kupitia Baraza la Michezo la Taifa na vyombo vingine vya michezo vya kitaifa itatayarisha mafunzo ya nadharia juu ya maadili

ya nchi kwa wanamichezo wakati timu zinapokuwa katika maandalizi kwa ajili ya uwakilishi wa Wilaya Mkoa na Taifa;

(3) Wachezaji lazima watambue kwamba ni sifa na heshima kubwa kuchaguliwa kwenye timu za Wilaya Mkoa na Taifa. Lazima wajenge nidhamu nzuri ya hali ya juu na tabia nzuri pia;

(4) Ili kumsaidia mchezaji kujenga nidhamu ya kimchezo zitakuwepo sheria na kanuni, za michezo ambazo zitamtawala mchezaji awapo kambini, mazoezini na wakati wa mashindano. Baraza la Michezo la Taifa litashirikiana na vyama vya michezo vya Taifa kutunga sheria na kanunui hizo;

(5) Mchezaji anayewakilisha wilaya, mkoa na taifa ahesabiwe yuko kazini. Kwa hiyo atapewa haki zake zote kulingana na Kanuni za Utumishi endapo ni mfanyakazi.

## 10.0 HUDUMA ZA WANAMICHEZO:

Katika suala zima la kuwathamini wanamichezo wetu, zitatolewa huduma muhimu ambazo zitaimarisha afya zao, zitakuza ari ya kucheza, kukuza ufundi wa binafsi na wa timu na kuwatia hamasa ya kuzidi kupenda kucheza hususani katika timu ya taifa.

Wizara yenye dhamana ya michezo kwa kupitia Baraza la Michezo la Taifa na vyombo vyote vinavyosimamia michezo itaweka utaratibu utakaowezesha huduma hizo kutolewa. Huduma zifuatazo zitapewa kipaumbele:-

## 10.1 Huduma za Afya:

(a) Mchezaji lazima achunguzwe afya yake na kuwekewa kumbukumbu zote za kiafya kwa kipindi chote;

(b) Wachezaji wawapo kambini lazima wahudumiwe na daktari mwenye taaluma ya tiba ya wanamichezo;

(c) Utaratibu wa matibabu kwa wanamichezo ujumuishe mafunzo juu ya athari za kutumia madawa ya kuongeza nguvu wakati wa michezo. Aidha uwekwe utaratibu wa kuchunguza wachezaji dhidi ya utumiaji wa madawa hayo.

## 10.2 Huduma ya Chakula:

Wachezaji wawapo kambini, mazoezini na kwenye mashindano, lazima wapatiwe malazi mazuri na chakula cha kutosha chenye viini vyote vinavyohitajika katika kujenga mwili na afya bora.

## 10.3 Motisha Mbalimbali:

Motisha zinazostahili kutolewa kwa wachezaji ni pamoja na posho za kujikimu, tuzo kwa kuliletea taifa sifa na mafunzo ya hali ya juu katika taaluma ya mchezo unaohusika. Aidha wanamichezo wastaafu watapewa kipaumbele katika kupewa nafasi za mafunzo ya juu na watatambuliwa kitaifa

Wachezaji watapatiwa vifaa muhimu vya mazoezi na vya mashindano. Aidha wataelimishwa juu ya umuhimu wa kuvitunza.

### 10.4 Huduma ya Bima:

Wachezaji wa timu za taifa lazima watawekewa bima katika kipindi chote cha mashindano yanayohusika. Aidha vilabu vya michezo vitawawekea bima wachezaji wao.

## 11.0 VYOMBO VYA HABARI KATIKA KUENDELEZA MICHEZO:

Ili umma uweze kushiriki kikamilifu katika michezo, lazima uelimishwe na kuhamasishwa, kwa:-

(a) kushirikisha vyombo vya habari katika kutoa makala maalum za kielimu kaika michezo;

(b) Kuwaelimisha waandishi wahabari katika taaluma ya michezo ili habari zinazotolewa ziwe sahihi;

(c) Kuhakikisha kwamba habari za michezo zenye faida kwa wanamichezo zinapatikana wakati wote;

(d) Kuhakikishwe kuwa waandishi wa habari za michezo wanapewa nafasi ya kujifunzia taaluma ya uandishi wa michezo.

## 12.0 UGHARAMIAJI WA MICHEZO:

Aina zote za michezo zinahitaji fedha za kuiendesha. Ili kupata fedha za kutosha kuigharamia itabidi vyombo mbalimbali vishirikiane. Hii ni pamoja na
Serikali Kuu, Serikali za Mitaa/Miji, Mashirika ya Umma, Makampuni hata watu binafsi wapenzi na wakereketwa wa michezo katika maeneo yao.

Kwa mujibu huo:-

(a) Kila ngazi ya serikali itabidi kutenga fedha za kugharamia shughuli mbalimbali za michezo kila mwaka ;

(b) Wizara yenye dhamana ya michezo itashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuwashawishi wafanya biashara kuagiza kwa wingi vifaa vya michezo. Aidha Serikali itahakikisha kwamba vifaa vya michezo vinatengenezwa hapa nchini;n

(c) Vifaa vya michezo pamoja na mali ghafi ya kutengeneza vifaa hivyo vitozwe kodi nafuu.

(d) Vifaa vya michezo vinavyotolewa kama zawadi kwa wanamichezo visitozwe kodi;

(e) Gharama za matunzo ya viwanja vya michezo zitokane na mapato yanayotokana na amatumizi ya viwanja hivyo. Mifuko maalum kama vile revolving fund itaanzishwa;

(f) Fedha za kugharamia maandalizi ya Timu mbalimbali:-

(i) Litakuwa ni jukumu la serikali na vyombo vinavyosimamia michezo kuwahamasisha wananchi kuchangia fedha za kugharimia na kuandaa timu zitakazoshiriki mashindano mbalimbi mbali;

(ii) Gharama za maandalizi ya timu za taifa zitaratibiwa na vyombo vyenye dhamana ya michezo. Aidha vyombo hivyo vitaweka taratibu za kushirikisha sekta mbalimbali kuchangia ghrama hizo;

(iii) Baraza la Michezo la Taifa litahakikisha kuwa asilimia ya mapato ya viingilio katika viwanja vya michezo inaongezwa kuliko ilivyo sasa ili kugharamia maandalizi ya timu za taifa na kuchangia maendeleo ya jumla ya michezo mbalimbali.

(g) Mafunzo ya wataalam yatagharimiwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazohusika.

## International Charter of Physical Education and Sport

### Preamble

The General Conference of the United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization, meeting in Paris at its twentieth session, this twenty-first day of November 1978, Recalling that in the United Nations Charter the peoples proclaimed their faith in fundamental human rights and in the dignity and worth of the human person, and affirmed their determination to promote social progress and better standards of life, Recalling that by the terms of the Universal Declaration of Human Rights, everyone is entitled to all the rights and freedoms set forth therein without discrimination of any kind as to race, colour, sex, language, religion, political or other opinion, national or social origin, property, birth or other consideration,

Convinced that one of the essential conditions for the effective exercise of human rights is that everyone should be free to develop and preserve his or her physical, intellectual and moral powers, and that access to physical education and sport should consequently be assured and guaranteed for all human beings,

Convinced that to preserve and develop the physical, intellectual and moral powers of the human being improves the quality of life at the national and the international levels.

Believing that physical education and sport should make a more effectiv contribution to the inculcation of fundamental human values underlying the full development of peoples,

Stressing accordingly that physical education and sport should seek to promote closer communion between peoples and between individuals together with disinterested emulation, solidarity and fraternity, mutual respect and understanding, and full respect for the integrity and dignity of human beings.

Considering that responsibilities and obligations are incumbent upon in the industrialized countries and the developing countries alike for reducing the disparity which continues to exist between them in respect of free and universal access to physical education and sport,

Considering that to integrate physical education and sport in the natural environment is to enrich them and to inspire respect of the earth's resources and the concern to conserve them and use them for the greater good of humanity as a whole.

Taking into account the diversity of the forms of training and education existing in the world, but noting that, notwithunderstanding the differences between national sports structures, its clearly evident that physical education and sports and confined to physical well-being and health but also contribute to the full and well-balanced development of the human being,

Taking into account, furthermore the enormous efforts that have to be made before the right to physical education and sport can become a reality for all human beings,

Stressing the importance for peace and friendship among peoples of co-operation between the international governmental and non-governmental organizations responsible for physical education and sport,

Proclaims this International Charter for the purpose of placing the development of physical education and sport at the service of the human progress, promoting their development, and urging governments, competent non-governmental organizations, educators, families and individuals themselves to be guided thereby, to disseminate it and to put it into practice.

**Article I:** The practice of physical education and sport is a fundamental right for all

1.1. Every human being has a fundamental right of access to physical education and sport, which are essential for the full development of his personality. The freedom to develop physical, intellectual and more powers through physical education and sport must be guaranteed both within the educational system and in other aspects of social life.

1.2 Everyone must have full opportunities, in accordance with his national tradition of sport, for practicing physical

education and sport, developing his physical fitness and attaining a level of achievement in sport which corresponds to his gifts.

1.3 Special opportunities must be made available for young people, including children of pre-school age, for the aged and for the handicapped to develop their personalities to the full through physical education and sport programmes suited to their requirements.

**Article 2:** Physical education and sport form an essential element of lifelong education in the overall education system.

2.1 Physical education and sport, as an essential dimension of education and culture, must develop the abilities, will-power and self-discipline of every human being as a fully integrated member of society. The continuity of physical activity and the practice of sports must be ensured throughout life by means of a global, lifelong and democratized education.

2.2. At the individual level, physical education and sport contribute to the maintenance and improvement of health, provide a wholesome leisure-time occupation and enable man to overcome the drawbacks of modern living. At the community level, they enrich social relations and develop fair play, which is essential not only to sport itself but also to life in society.

2.3 Every overall education system must assign the requisite place and importance to physical education and sport in order to establish a balance and strengthen links between physical activities and other components of education.

**Article 3:** Physical education and sport programmes must meet individual and social needs

3.1 Physical education and sport programmes must be designed to suit the requirements and personal characteristics of those practicing them, as well as the institutional, cultural, socio-economic and climatic conditions of each country. They must give priority to the requirements of disadvantaged groups in society.

3.2 In the process of education in general, physical education and sport programmes must, by virtue of both their content and their timetables, help to create habits and behaviour patterns conducive to full development of the human person.

3.3 Even when it has spectacular features, competitive sport must always aim, in accordance with the Olympic ideal, to serve the purpose of educational sport, of which it represents the crowning optima. It must in no way be influenced by profit-seeking commercial interests.

**Article 4** Teaching, coaching and administration of physical education and sport should be performed by qualified personnel.

4.1 All personnel who assume professional responsibility for physical education and sport must have appropriate qualifications and training. They must be carefully selected in sufficient numbers and given preliminary as well as further training to ensure that they reach adequate levels of specialization.

4.2 Voluntary personnel', given appropriate training and supervision, can make an invaluable contribution to the comprehensive development of sport and encourage the participation of the population in the practice and organization of physical and sport activities.

4.3 Appropriate structures must be established for the training of personnel for physical education and sport. Personnel who have received such training must be given a status in keeping with the duties they perform.

**Article 5** Adequate facilities and equipment are essential to physical education and sport

Adequate and sufficient facilities and equipment must be provided and installed to meet the intensive and safe participation in both in-school and out-of school programmes concerning education and sport.

This incumbent on governments, public authorities, schools and appropriate private agencies, levels to join forces and plan together so as to provide and make optimum use of installations, and equipment for physical education and sport.

It is essential that plans for rural and urban development include provision for long term the matter of installations, facilities and equipment for physical education and sport, taking in account the opportunities offered by the natural environment.

**Article 6** Research and evaluation are indispensable components of the development of physical education and sport.

Research and evaluation in physical education and sport should make for the progress of all kinds of sport and help to ring about an improvement in the health safety of participants as well training methods and organization and management procedures. The education system will benefit from innovations calculated to develop better teaching methods and standards of finance.

Scientific research whose social implications in this sphere should not be overlooked, must be granted in such a way that it does not allow of improper applications to physical education and sport.

**Article 7.** Information and documentation help to promote physical education and sport

The collection, provision and dissemination of information and documentation on physical education and sport constitute a major necessity. In particular, there is a need to circulate information results of research and evaluation studies concerning programmes, experiments and activities.

**Article 8**. The mass media should exert a positive influence on physical education and sport.

Without prejudice to the right of freedom of information, it is essential that everyone involve in mass media be fully conscious of his responsibilities having regard to the social importance, the Gnostic purpose and the moral values embodied in physical education and sport.

Relations between those involved in the mass media and specialists in physical education and sport must close and based on mutual confidence in order to exercise a positive influence on physical education and sport and to ensure objective and well-founded information. Training of personnel for the media may include elements relating to physical education and sport.

**Article 9** National Institutions play a major role in physical education and sport.

It is essential that public authorities at all levels and specialized non-governmental bodies encourage those physical education and sport activities whose educational value is most evident.

9.1. Action shall consisting in enforcing legislation and regulations, providing materials assistance and acting all other measures of encouragement, stimulation and control. The public authorities will ensure that such fiscal measures are adopted as may encourage these activities.

9.2. It is incumbent on all institutions responsible for physical education and sport to promote a resistant, overall and decentralized plan of action in the framework of lifelong education so as to for continuity and co-ordination between compulsory physical activities and those *practiced and spontaneously.*

**Article10** International co-operation is a prerequisite for the universal and well-balanced promotion of physical education and sport.

10.1 It is essential that States and those international and regional intergovernmental and non-governmental organizations in which interested countries are represented and which are responsible for physical education sport give physical education and sport greater prominence in international bilateral and multilateral co-operation.

10.2 Internal co-operation must be prompted by wholly disinterested motives in order to promote and stimulate endogenous development in this field.

10.3 Through cooperation and pursuit of mutual interestes in the universal language of physical education and sport, all peoples will contribute to the preservation of lasting peace, mutual respect and friendship and will thus create a propitious climate for solving international problems. Close collaboration between all interested national and international governmental and non governmental agencies, based on respect for the specific competence of each, will necessarily encourage the development of physical education and sport throughout the world.